

BARUA YA WAZI KWA MUHESHIWA SHEIKH SÂLIH AS-SUHAYMÎ KUTOKA KWA SHEIKH ALI HASAN AL-HALABI (حفظهما الله)

15 April, 2015 | Posted by [Salafibayaan](#) | [Clarifications](#) | 605 views



Bismillaah ir-Rahmaan ir-Raheem,

As-salaamu alaykum wa rahmatullaahi wa barakatuh,

Amma ba'd:

Baadhi ya mazungumzo yaliyonasibishwa kutoka kwa Sheikh Sâlih as-Suhaymî yamesambazwa kupitia kwenye matangazo ya ki-jamii, katika kanda kwa jina la 'Kikao pamoja na ndugu wa ki-Marekani', ambapo Sheikh Suhaymî aliposema (katika dakika ya 18 na sekunde 20):

“Mimi najuwa yakwamba wamefikia kiwango cha wazushi, ‘Ali Hasan na Abu’l Hasan.’

Na baada ya dakika ishirini na sekunde 42:

“Mimi nambaddi’ (nachukuwa hatua za kumfanya kuwa ni mzushi), ‘Ali Hasan, namuona kuwa yeye ni mzushi, na vilevile Abu’l Hasan, namuona kuwa ni mzushi.”

Mimi nasema (Sheikh ‘Ali Hasan) katika kutoa maoni yangu:

Natumai yakwamba Sheikh Suhaymî (*hafidhahullâh*) anaweza kunibainishia mimi kwa dalili, mtazamo na sababu za tabdî' yake juu yangu, ili nipate kutubia, iwapo maneno yake ni ya ukweli. Ama kuhusu kujitegemeza ovyo juu ya “Bwana huyu amesema..., Bibi huyu asema...” na “Yasemekana ati...”, basi huu sio Usalafiyyah ambao tuliokuja kuujuwa kutoka kwa wanavyuoni wetu wakubwa. Natumai yakwamba kila aliye na mafungamano na Sheikh huyu kwa njia yoyote iwayo anaweza kumfikilizia ujumbe wangu kwake, kabla mimi sijafa au yeye hajafa. Mimi niko tayari kikamilifu kuonana na muheshimiwa Sheikh wakati wowote au mahali popote atakapo yeye, kwa uwezo wa Allâh. Namuomba Allâh atuja'aliye sote kufuzu katika maisha ya hapa duniani na kesho akhera.

Yamefasiriwa na al-Akh Abu Farida
THE QUR'AN AND SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA
QSSEA, MOMBASA

[1] Kutoka: <http://kulalsalafiyeen.com/vb/showthread.php?t=64620>

Tarehe 14th April 2015.